

MAJILIO 2026 – WIKI YA 4

STAAJABU!

Kulitumaini Kusudi la Mungu kwa Ulimwengu Mzima

Luka 1:26-45



**“Kwa maana jinsi hii Mungu
aliupenda ulimwengu, hata
akamtoa Mwanawe pekee,”**

Yohana 3:16 (SRUV)



Leo tunawasha mshumaa wa UPENDO.

**Mariamu alikubali mpango wa Mungu,
na imani yake ilibadilisha ulimwengu.**



Tunawasha mshumaa huu kwa ajili ya mataifa ambayo bado yanasubiri kusikia kuhusu upendo wa Mungu.

Kwa ajili ya wamisionari wanaovuka mipaka ya tamaduni ili kuushiriki upendo huo, kwa ajili ya makanisa yanayowakaribisha wageni, na kwa ajili ya waumini wanaowapenda adui zao.



**Kama Mariamu, tumeitwa
kumtumaini Mungu na kushiriki
katika kazi yake ulimwenguni.**

**Tukubali kushiriki katika utume wake na kuupeleka
upendo wake hadi miisho ya dunia.**



**Mungu wa upendo, tunakushukuru
kwa kumtuma Yesu ili kutuonyesha
maana halisi ya kupenda.**

Tupe nguvu za kupenda kwa ujasiri, kuvuka mipaka na kuudhihirisha
moyo wako kwa kila taifa. Mshumaa huu utukumbushe kwamba
upendo wako ni kwa ajili ya watu wa mataifa yote.

Amina.



